# THE TIMER NATIONAL SERIES
## JUNIOR SCHOOL ASSESSMENTS 2024
## SHUGHULI ZA KISWAHILI {8}

JS 0032024

JINA LA MTAHINIWA: ..........................................................................................

NAMBARI YA UTAHINI: .......................................................................................

JINA LA SHULE: ................................................... TAREHE: ..................................

**ZOEZI 1 : KUSOMA**

***KUSOMA KWA UFAHAMU***

***Soma ufahamu ufuatao kisha ujibu maswali.***

Katika nchi ya Ustawi, wananchi wengi walipata ari ya kujiandalia maisha bora ya baadaye. Walithamini sana mustakabali wa wana wao. Ili kufanikisha haya, waliunda vyama vya ushirika. Wananchi walipata mikopo isiyo na riba kubwa. Wananchi wa Ustawi walipambana kwa hali na mali kuimarisha hali yao ya maisha. Muda si muda, vyama vikastawi. **Fedha walizopata zilivunja nguu na milima ikalala**. Kwa wananchi wengi wa Ustawi, biwi la mashaka tipitipi liliondolewa na baadaye wakaanza kuishi kama watu. Usimamizi mzuri wa vyama ulizaa matunda yaliyowafaa wananchi wote.

Baada ya uchaguzi wa wanachama, uongozi mpya ulishika hatamu. Lakini kumbe ngoma ya wana haikeshi! Viongozi waliojawa na tamaa walivuruga usimamizi wa vyama. Ahadi za kuendeleza na kuboresha vyama vya ushirika zilitupwa katika jaa! Walitumia hila kujipa mikopo mikubwa ambayo hawakulipa. Matumizi yasiyo na mipango yaliwekwa katika ratiba. Wengine walipora mali ya wanachama. Kutokana na wizi na wanachama kuchezeshwa ngoma, vyama vilianza kulegalega. Ukweli wa wakubwa kuwameza wadogo ulianza kubainika. Wanachama walijuta kwa kutojua kuwa paka hawekewi maziwa kulinda.

Wananchi waliingiwa na kiwewe. Waliogopa kurudia umaskini wa hapo awali. Waliililia serikali, nacho kilio chao kikasikika. Serikali iliagiza vyama vyote visajiliwe na kuunda katiba. Sheria aidha iliweka vigezo vya watu wanaopaswa kuongoza vyama. Miongoni mwa vigezo hivyo vilikuwa ni elimu, tajriba, maadili na uwajibikaji. Kwa amri ya serikali, madaftari ya uhasibu wa vyama yalikaguliwa. Waliopatikana na hatia **walikula kalenda**. Bunge la nchi lilitunga sheria nzuri zilizolenga kulinda vyama vya ushirika. Mapato ya vyama yakaanza kuimarika.

1. Kuundwa kwa vyama vya ushirika kulikuwa na umuhimu gani kwa wananchi wa Ustawi? **(alama 1)**

______________________________

______________________________

2. Eleza maana ya kidokezi kilichoangaziwa katika paragrafu ya kwanza. **(alama 2)**

______________________________

______________________________

______________________________

3. Ni nini hasa kilichowaondolea wananchi wa Ustawi mashaka yaliyowazonga? **(alama 1)**

______________________________

______________________________

4. Uongozi mpya uliwaletea wanachama wa vyama vya ushirika maafa gani? **(alama 1)**

______________________________

______________________________

5. Maovu gani makuu katika jamii yamepewa kipaumbele katika aya ya pili? **(alama 1)**

______________________

6. Ukweli wa methali "**Tamaa mbele mauti nyuma**" unajitokeza vipi katika makala haya? **(alama 2)**

______________________

______________________

7. Badala ya kusema **walikula kalenda**, mwandishi angesemaje? **(alama 1)**

______________________

8. Kimsingi, wanachama wa vyama vya ushirika walinufaika vipi na mchango wa serikali? **(alama 2)**

______________________

______________________

**ZOEZI 2: UFUPISHO**

Magari madogo madogo ya uchukuzi wa umma yenye magurudumu matatu yameanza kuwa namna maarufu ya usafiri. Wanaoabiri magari ili kusafiri huyachangamkia na kuyafurahia kwa ajili hayabebi watu wengi; kwa hivyo, kuna mzunguko mzuri wa hewa.

Hayo tukiyaachilia mbali, magari haya hutoza hela nafuu za usafiri kwani, mara kwa mara, huwa hayasafiri masafa marefu. Kando na hayo, ingawa magari haya yana uwezo wa kusafiri kwa kasi ya hadi kilomita sitini na tano kwa saa, huendeshwa kwa mwendo wa kobe ili kusitokee ajali yoyote barabarani.

9. Fupisha aya ya kwanza kwa maneno yasiyozidi ishirini. **(alama 2)**

______________________

______________________

______________________

______________________

______________________

10. Badala ya kutumia hela za usafiri, kwa neno moja mwandishi angetumia neno lipi? **(alama 1)**

______________________

11. Habari kuu katika aya ya kwanza ni gani? **(alama 2)**

______________________

______________________

12. Kwa mujibu wa aya ya pili, kwa ufupi, dondoa sababu za watu kuyapenda magari yaliyotajwa. **(alama 2)**

______________________

______________________

______________________

**ZOEZI 3: SARUFI** **(alama 5)**

_____13_____ ni chombo maarufu sana katika matilaba ya kupashana habari. Hutumika kwingi kuliko magazeti na runinga ambazo zimezoeleka sana katika _____14_____ mikubwa mikubwa. Hupatikana kwa miundo na aina mbali mbali, tena, zipo za bei nafuu zaidi hadi shilingi _____15_____. Zipo zilizo ghali zaidi. _____16_____, ibainike kuwa simu zizo hizo huwa na manufaa na _____17_____ pia.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 13. | A. Televisheni | B. Redio | C. Rununu | D. Majarida |
| 14. | A. mitaa | B. mipaka | C. mito | D. miji |
| 15. | A. elfu moja | B. thelathini | C. elfu tisini | D. sitini |
| 16. | A. Kwa hivyo | B. Hata hivyo | C. Hivyo basi | D. Sasa basi |
| 17. | A. madhila | B. ubora | C. madhara | D. uzuri |

18. Iandike sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa: **(alama 1)**
**"Nitakibeba kikapu changu na kuelekea sokoni," Mama akasema.**

______________________________

______________________________

19. Kanusha sentensi ifuatayo kwa usahihi: **(alama 1)**
**Waliocheza vizuri walituzwa.**

______________________________

20. **Nilimwona <u>ndege</u> mkubwa angani.** Andika ukubwa wa neno lililopigiwa mstari. **(alama 1)**

______________________________

Tambua aina hizi za sentensi. **(alama 2)**

21. Mtoto anacheza

______________________________

22. Nilimwendea nikamwita.

______________________________

23. **Nyanya alisomewa barua na Farashuu.** Iandike upya wentensi hii ukianza kwa neno Farashuu. **(alama 1)**

______________________________

______________________________

**Kamilisha jedwali lifuatalo.** **(alama 2)**

| | Neno | Kinyume |
|---|---|---|
| 24. | Mnene | ________ |
| 25. | ________ | Mgeni |

Andika nomino moja katika kila ngeli. **(alama 2)**

26. KI - VI ____________________

27. LI - YA ____________________

## <u>ZOEZI LA 7: FASIHI - Wema Hauozi</u>

28. Kwa kurejelea tamthilia ya Wema Hauozi, taja sababu kuu iliyomfanya mabula kumwita mkewe Mishi alipokuwa amelala juu ya sofa kuukuu. **(alama 1)**

______________________________

______________________________

29. **".... Sikiliza Mishi nikuambie. *It is just a matter of time na mimi nitakuwa where I belong*"** Tambua mbinu iliyotumika katika dondoo hii. **(alama 1)**

______________________________

______________________________

30. **Mabula ni mtu anayetumia visingizio ili kuuziba udhaifu wake.** Fafanua kauli hii kwa ufupi ukirejelea tamthilia ya Wema Hauozi. **(alama 2)**

______________________________

______________________________

______________________________

31. Mwanzoni mwa tamthilia ya Wema Hauozi, familia ya Mabula na Mishi inaonekana kuogelea katika bahari ya umaskini. Thibitisha kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya Wema Hauozi. **(alama 1)**

______________________________

______________________________

## ZOEZI 8: NOVELA

Mimi na wazazi wangu tulikuwa tukiishi Kisamale. Hapo ndipo palikuwa na mji wetu. Nilizaliwa hapo, nikakulia hapo hadi kujiunga na shule ya msingi. Udogoni, nilikuwa nikitangamana na kila mtu bila kuwa na ubaguzi wa kimbari wala kikabila. Wakati huo niliamini kwamba binadamu wote tulikuwa sawa.

Muda ulisonga huku tukiendelea na shughuli zetu. Uvumi wa vurugu ulitulia kwa muda na maisha yakarejelea hali yake ya kawaida. Binafsi nilishukuru sana. Nilikuwa na marafiki wengi Walanga na Wareba. Sikutaka kukosana nao. Ningekosana nao, ningecheza mpira na nani? Shuleni ningesoma vipi bila marafiki? Sikutaka mzozo baina yetu. Nilishukuru kuona kuwa amani ilirejea na watu waliendelea na shughuli zao za kawaida. Wakristo walienda makanisani nao Waislamu wakaenda misikitini. Wanasiasa walifanya siasa zao nao wakulima wakapanda mashambani mwao. Mavuno yalinawiri na kuvunwa. Jua lilichomoza mashariki na kutua magharibi. Kuku waliotaga mayai waliyaatamia na kuangua. Wa kunadi sala katika misikiti walinadi. Ndege wa mwituni waliimba. Upepo wa kusi ulivuma. Jua liliwaka na mvua kunyesha. Watu walizaliwa na wengine wakafa. Maji ya bahari yalijaa na kupwa. Siku zilisonga kama kawaida.

Ghafla bin vuu, uvumi ulibisha hodi tena kwa kishindo. Mara hii ulikuwa na kishindo kikuu. Kila mtu aliyeusikia alifadhaika. Watu wengi walitapatapa kwa woga.

"Ala! Umerudi tena huu uvumi jamani," baba alimweleza mama jioni moja.

"Potelea mbali. Si kweli. Nikwambie mara ngapi ndipo unisikie? Hizo ni kelele za chura zisizomzuia tembo kunywa maji," mama alimwambia baba.

"Ninapendekeza mhamie Azania au jamhuri ya Demokrasia ya Tereka kwa muda," baba alimshauri mama yangu.

"Sioni haja ya kuwa na wasiwasi namna hii. Habari hizi zitapita kama zilivyopita zile za awali," mama aliendelea kupinga ushauri ya baba.

Laiti angetambua mapema ukweli wa maneno ya baba na kuyatilia maanani, mambo hayangetumbukia nyongo kama yalivyotokea. Labda tungehamia nchini Azania au Jamhuri ya Demokrasia ya Tereka kama alivyopendekeza baba yangu tungekuwa salama. Lakini mama yangu alikuwa mshindani mno. Alikataa katakata kusikia ushauri aliopewa.

**32.** Ni kwa nini mwandishi hakutaka kukosana na Walanga na Wareba? **(alama 1)**

______________________________

______________________________

______________________________

**33.** Msimulizi anamwuliza nani maswali yaliyo katika aya ya pili? **(alama 1)**

______________________________

**34.** Hoja kuu inayojitokeza katika aya ya pili ni ipi? **(alama 1)**

______________________________

______________________________

______________________________

**35.** Ni kwa nini mama hakupendezwa na wazo la baba la kuhamia Azania au Jamhuri ya Demokrasia ya Tereka? **(alama 1)**

______________________________

______________________________